

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

FURSA YA KUSHIRIKI KWENYE TUZO ZA
"2024 EQUALS IN TECH AWARDS"

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa imepokea taarifa ya fursa za tuzo zinazojulika kama "2024 EQUALS in Tech Awards" kutoka Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU). Tuzo hizi zina lengo la kutambua juhudi na mipango mbalimbali, miradi, mashirika na taasisi zinazofanya kazi ili kupunguza wigo wa uwiano wa kijinsia wa kidijitali. Tuzo hizo hutolewa na washirika wa "EQUALS" ikiwemo ITU.

Kila mwaka, washirika tajwa huandaa tuzo hizi kwa miradi na mipango ya kujitolea na bunifu zinazolenga kuwapa wanawake na wasichana fursa za kushiriki kwenye shughuli za kimtandao, ujuzi muhimu wa kidijitali, na fursa za kazi katika teknolojia. Aidha tuzo hizi hutambua na kuenzi makundi ya washirika wa kimataifa na kutoka sekta mbalimbali wenye malengo ya kuhakikisha usawa wa ushiriki wa wanawake na wasichana katika enzi ya kidijitali.

Tuzo hizi zimegawanyika katika makundi matano: Upatikanaji wa huduma, Ujuzi, Uongozi katika Teknolojia, Uongozi katika Biashara Ndogo, na Utafiti. Washindi watafaidika na kujiunga na jumuiya kimataifa na kupata usaidizi na kupanua mitandao yao.

Ili kushiriki kwenye tuzo hizi, tafadhali tembele tovuti ya <https://www.equalsintech.org/awards> ili ujaze fomu na kuwasilisha maombi. Aidha mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe **1 Septemba, 2024** Saa **6:00 usiku** kwa saa za Afrika Mashariki.

Imetolewa tarehe **27 Julai, 2024**

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.

Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10

Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz